TransformationSeries#02

# MBINU 8 ZA KUKUSAIDIA KUFAULU MITIHANI YAKO KWA KIWANGO CHA JUU

**“Si utayari wa kushinda unaohitajika – huo kila mmoja anao. Ni utayari wa kujiandaa kushinda ndiyo unaohitajika” ~ Paul “Bear” Bryant**

Joel Arthur Nanauka.

**© 2020 Joel Arthur Nanauka**

Haki zote zimehifadhiwa. Huruhusiwi kunakili, kudurufu au kutumia sehemu ya kitabu hiki bila idhini ya mwandishi. Kufanya hivyo itakuwa ni ukiukwaji wa haki za mwandishi, na ukiukwaji wa taratibu hii unaweza kupelekea mashitaka toka kwa waandaaji wa kazi hii.

JOEL ARTHUR NANAUKA

Dar-Es-Salaam, Tanzania. East Africa

Simu: +255 756 094875/0745 252 670

Barua pepe: jnanauka@gmail.com

Tovuti: www.joelnanauka.com

Kimepangiliwa na

Infinite Press

Contact us: Lights On
+255 757400948/+255 620 319 485.
Email: praisearnold.pa@gmail.com

# *Yaliyomo*

Utangulizi …………………………………………......… 3

1: Mkakati wa kusoma……………………………….. 5

2: Mkakati wa maandalizi ya vifaa vinavyohitajika…. 10

3: Mkakati wa kurudia kusoma…………………….… 13

4: Mkakati wa kulala (kupumzika)………………...… 17

5: Mkakati wakupima uwezo wako……………...…... 19

6: Mkakati wa makundi ya kujadiliana…………….... 22

7: Mkakati wa kuchunguza mpangilio wa mtihani...… 28

8: Mkakati wa kukumbuka………………..………… 31

Hitimisho ………………………………………………. 36

Kuhusu mwandishi…………………………...……… 37

# *Utangulizi*

Tofauti ya alama za ufaulu wanafunzi wanazopata zinaanzia katika kujindaa kwao. Hii ni rahisi tu kuwa kama hujui namna ya kujiandaa kwa mtihani wako utakuwa muda wote ni mtu wa kupoteza alama katika mtihani wako.

Muda wako wa kujiandaa ndio muda wako wa kushinda, kufamu nini cha kufanya katika kujiweka sawa kwa ajili ya mtihani wako kunatengeneza tofauti kubwa sana katika ufaulu wako. Ni bahati mbaya sana tumefundishwa namna ya kujibu maswali shuleni lakini hakuna anayetufundisa namna ya kujiandaa ili kujibu vyema maswali.

Haijalishi ni kwa namna gani mpiganaji wa ngumi yuko vizuri akiacha kufanya maandalizi na mazoezi kwa ajili ya ulingo ujao anajitengenezea kushindwa, vivyo hivyo kama unatamani kufaulu haiwezekani bila kufanya maandalizi kwa ajili ya mitihani yako.

Katika maisha kuna kanuni moja inaitwa *“Winning edge”* Hii kanuni, inasema kwamba “tofauti ndogo katika uwezo inaweza kubadilishwa na kuwa tofauti kubwa sana katika matokeo”. Hii inamaanisha nini? Kama utakuwa vizuri japo kidogo katika eneo fulani la muhimu katika masomo yako, inaweza kuleta ongezeko katika alama zako.

Ki ukweli unaweza kuwa kwenye ukingo wa hatua moja zaidi katika taaluma yako, katika wakati huu ni kwa kujifunza na kufanya mazoezi sana ya kitu kipya na tofauti kama ulivyofanya kabla.

Kama katika mashindano ya farasi, farasi anayeshindwa kwa kutanguliza pua yake tu anapata zawadi mara kumi zaidi ya Yule aliyekuwa wa pili yake, hata kama tofauti yao ilikuwa ni pua tu, au inchi kadhaa tu.

Vivyo hivyo kinachoweza kuwatofautisha watu katika ufaulu wao siyo kazi kubwa ya maandalizi lakini ni ile kidogo lakini yenye maarifa ya kutosha. Jambo jema ni kuwa leo unakwenda kufahamu siri katika maisha yako ambazo zitabadilishha sura na taswira ya taaluma yako.

Wale wote waliofanikiwa katika mitihani yao kwa alama za juu sana wametumia kanuni hizi nane. Mimi mwenyewe nimezitumia na kuwafundisha watu na wamerudi na kuthibitisha zinafanya kazi. Unaweza jisajili kuwa mmoja wa wanafunzi bora ambao wanafaulu mitihani yao kwa ufaulu mzuri kwa kujifunza hizi kanuni 8 za mkakati wa nguvu.

# 1.

# Mkakati wa kusoma

*"Ufahamu uwezo wako wa kusoma na uufuate huo, usiwe mwoga wa watu wanaojaribu kukutisha kwa staili zao za kusoma."*

Jinsi unavyopanga vitu au agenda za kusoma inahusika sana katika kukusaidia katika ufaulu wa mitihani. Naanza kwa kusema mkakati wa kusoma unatakiwa kuwa tofauti wakati unakaribia mitihani na wakati ambao uko mbali kuianza mitihani.

Katika hii pointi ni muhimu kufahamu kuwa kama unasoma na huna ratiba yako mwenyewe ya kujisomea hiyo ni sababu tosha ya kukurudisha nyuma katika ufaulu. Ninapendekeza kwamba kabla hujaendelea na sura nyingine kaa chini na utumie hizi siri utakazopata katka pointi hii kuandaa mpango mkakati wako wa kusoma.

Siri ya kuwa na mkakati wa kusoma au ratiba ni kujipa nidhamu na mpango mzuri ambao utakusaidia kutunza muda katika masomo yako. Zaidi, hii itakusaidia kuwa

makini sana, Kama hujawahi kuwa na ratiba yako, unapaswa kuwa nayo sasa.

***Mkakati wa kusoma unahusisha yafuatayo*:**

**a)** ***Nini cha kusoma*:** Tumia muongozo wa kozi yako na andaa orodha ya vitu ambavyo unatakiwa kuwa unavifahamu kabla ya kukaa katika mitihani yako. Unahitaji kufanya uamuzi katika vitabu na notes ambazo unazihitaji kusoma kama moja ya mpango mkakati. Kila mara ambapo unafanikiwa kumaliza sura moja ya ulizoorodhesha, kuwa na namna ya kuziwekea alama kuwa hiyo tayari umeshasoma.

Unahitaji kuandaa notsi za muongozo wakati unasoma kwa sababu hii inaweza kuwa ni notsi nzuri za kufanyia marejeo kabla hujaingia katika chumba cha mitihani. Notes za kujiandalia mwenyewe zina nguvu sana za kuchangamsha kumbukumbu na kukuza uelewa zaidi ya ukitumia notes za mtu mwingine.

**b)** ***Wakati gani wa kusoma**:* Moja ya sehemu ya kufaulu mtihani ni kujua muda sahihi ambao kwako ni wakati ambao unaweza kuelewa vizuri kuliko muda mwingine wowote, tunaita “Your best active time” moja ya changamoto niliyopata wakati najiunga na Kibaha Sekondari ni kuona watu wakiamka usiku na kusoma hadi asubuhi.

Katika kujaribu kufanya wanachofanya wengine nikajribu na kuja kugundua kuwa kwangu ile staili ya kusoma hainifai. Kwa sababu hiyo nikaamua kurudi kwenye njia yangu ambayo nilikuwa nasoma mpaka usiku

sana na kisha nalala mpaka asubuhi na mara nyingi nilikuwa napata muda wa kupumzika mchana au jioni. Kwa vyovyote ni lazima ufahamu nguvu zako na uzifuate na usiwe na woga wa watu wanaojaribu kukutisha kwa staili zao za kusoma.

**c) *Unasomea wapi?*** Usomaji wako ni sababu nyingine ya kuongeza au kupunguza ufanisi na umahiri wako wa masomo. Kila mmoja ana mazingira fulani ya kwake na haya mazingira yanafanya kuwa rahisi kuelewa mambo mengi ya uliyosoma na kukusaidia kuwa na nguvu ya kusoma kwa muda wa kipindi kirefu bila ya kuchoka.

Nilipokuwa mwaka wangu wa pili katika chuo kikuu cha Dar es Salaam tulikuwa tumepangwa kufanyia mtihani katika maktaba ya chuo. Nilipokuwa naingia maktaba mhusika wa maktaba alinisimamisha na kuniulza "kwa nini unajaribu kuingia maktaba kupitia sehemu wanayotokea?" nikamjibu sijui kwa sababu hakuna alama yoyote kuwa hapa ndio wanatokea na akaniambia "wanafunzi wote wanajua inakuwaje wewe hujui, uko mwaka wa ngapi? Nikamwambia nipo mwaka wa pili na sijawahi kuja maktaba kujisomea kabla, akanijibu kwa mshangao, "Hii ni mpya". Na ni kweli ilikuwa ni mpya sio kwake tu lakini kwa yeyote atakayesikia hii.

Lakini ukweli wa hili ni kutokana na mazingira yangu ya kujisomea, wakati huo nilikuwa najisomea chumbani kwangu na huku nasikiliza miziki ya taratibu. Zaidi sana nilikuwa napenda kujipumzisha kila baada ya dakika 40 na hii ingekuwa usumbufu kama ningesomea maktaba.

Sijajua ni mandhari gani kwako ni mazuri kusoma lakini kila mmoja wetu ana mazingira yake, ambayo ukiyajua na

kuyatumia utaongeza uwezo wa kuelewa. Japo hii inaweza isifanye kazi kwa kila mtu lakini ni nzuri sana. Hi imetokana na utafiti uliofanywa na George Lozanov juu ya mazingira ya kusoma.

Katika tafiti yake alikuja kugundua kuwa muda mzuri wa kusoma ni pale ambapo ubongo wako wa kulia na wa kushoto unafanya kazi kwa pamoja. Kwa kawaida ubongo hufanya kazi kwa mapigo 14 kwa sekunde, Ukiwa umetulia au unatafakari ubongo unafanya kazi kwa mapigo 8 – 13 kwa sekunde. Wakati umetulia ni muda mzuri wa wewe kusoma.

Lozanov aligundua kuwa kama mtu atatulia, kwa taarifa zilizopo wakati miziki ya taratibu ikipigwa nyuma yake, ubongo wa kulia na kushoto hufanya kazi kwa pamoja na swala zima la kusoma linaenda kwa kasi sana. Katika mwaka wa 1979, Lozanov aliweza kufundisha darasa maalumu maneno mapya 3000, ambayo ni sawa na kuzungumza vizuri lugha ya kigeni, kwa siku moja. Miezi 6 baadaye wanafunzi waliweza kukumbuka asilimia 60% ya walichofundishwa, ambayo ukilinganisha na ukumbukwaji wa kawaida wa asimilia 10%.

**d)** ***Nani wa kusoma naye:*** Ni kawaida kujikuta tuna watu ambao huwa tunasoma pamoja. Kutokana na uzoefu marafiki tunaosoma nao tunajikuta tunao lakini sio kutokana na uchaguzi wetu. Lakini cha muhimu hapa ni kujua kuwa yeyote tunayeamua kuungana naye ana uwezo wa kuathiri taaluma yetu aidha kwa uzuri au kwa ubaya.

Katika kitabu chake “The slight edge” Jeff Olson alisema, “Jinsi tulivyo ni wastani wa watu sita ambao tupo karibu

nao”. Hii nadharia imefanya kazi katika taasisi nyingi na inafanya kazi hata katika taaluma. Unaweza kuchukua wastani wa rafiki zako sita na kujichunguza mwenyewe, utashangaa na matokeo yake na kugundua kuwa ndivyo ulivyo.

Rafiki zako katika kusoma watakuathiri unachosoma, vipaumbele vyako, uhudhuriaji wako darasani na hata mtazamo wako juu ya masomo na walimu wako. Si ajabu kuona rafiki yako anachukia hesabu na wewe ukajikuta kidogo kidogo unachukia hesabu pia. Athari za watu ambao tunaambatana nao katika masomo yetu ya kila siku imefafanuliwa pia katika mkakati wa sita (6) kuhusu makundi ya kujadili.

# 2.

# Mkakati wa maandalizi ya vifaa vinavyohitajika

*"Kama huwezi pata vitu vyako vya kusoma kwa dakika mbili, hii ina maana kuwa mpango wako ni mbovu, kama huwezi muelekeza mtu mahali husika ulipoweka kitabu na akakiona, hii inakuambia kuwa mpango wako mbovu ndiyo staili ya maisha yako."*

Ni kama katika ujenzi wa nyumba unahitaji maandalizi ya vitendea kazi bora na toshelevu, Vivyo hivyo katika kujitahidi kupata ufaulu mzuri katiak mitihai unahitaji maandalizi mazuri ya vitendea kazi vyote vinavyohitajika katika kusoma kwako kabla ya kukaa katika chumba cha mtihani.

Unahitaji kufahamu nini unahitaji kuwa nacho kuweza kutimiza ulichokuwa unataka kusoma. Kama tulivyoona katika makakati wa kusoma kuwa unahitaji kuwa na

muongozo wa kozi (yaani syllabus), hii itakupa uhakika kuwa umeshasoma sehemu zote ambazo zinahitajika kusomwa katika masomo yako. Muda mwingi ni vitabu, sura za kusoma na notes zilizopendekezwa na mwalimu wako. Katika uandaaji wa vitendea kazi unahitaji kuhakikisha kuwa una kila kitendea kazi kinachohitajika mkononi mwako. Acha kuwa mtu ambaye muda wote wewe ni kuazima kitabu na notes za kusoma. Hakuna kitu kinachokupa shida kama kutaka kusoma kitu fulani na kugundua kuwa huna mahali pa kusoma na unataka kuazima na kila unaye jaribu kuazima aidha anatumia au hana.

Katika uaandaji wa vitendea kazi ni muhimu kufahamu ni kipindi gani ambacho ulikikosa na nini unahitaji kujua kutoka kwao. Mara nyingine kipindi ulichokosa darasani kina vitu vingi katika mtihani wako wa mwisho (Ki ukweli kipindi kimoja kinaweza kikawa na swali ambalo linajitosheleza kwa uwingi mkubwa wa alama).

Mara zote unapokosa kipindi kwa sababu fulani, hakikisha una mpango mkakati wa ufuatiliaji ni nini wenzako wamejifunza na chukua notes kutoka kwao, pata kujua ni nini mwalimu amesisitiza na kama inawezekana pata mwenzako mmoja ambaye atakuelekeza kwa kifupi.

Kama tulivyosema katika mkakati wa kusoma, pata namna ya kuwa unaandika kwa kifupi vitu vyote muhimu ambavyo vitakusaidia unapofanya marudio na wakati wa kusoma. Hii itakuwa kama marejeo rahisi muda wowote ambao unataka kujiandaa na mtihani.

Zaidi ni kuwa sehemu ya mkakati wa Kuandaa vitendea kazi vya kusoma unahitaji kuwa makini. Hakikisha una

mahali maalumu pa kuweka vitu vyako vyote vya kusomea na unaweza weka alama ili iwe rahisi kuvijua kwa haraka. Kuna watu wengi ambao wanapoteza muda sana kutafuta vitabu na notes kutokana na mpango mbovu. Kama huwezi pata vitu vyako vya kusoma kwa dakika mbili, hii ina maana kuwa mpango wako ni mbovu, kama huwezi muelekeza mtu mahali husika ulipoweka kitabu na akakiona, hii inakuambia kuwa mpango wako mbovu ndiyo staili ya maisha yako.

Katika mpango wako ni muhimu pia kuweka rekodi ya nani ameazima vitu vyako. Kuna watu wengi wanaazimisha vitu vyao na wakati wanataka kutumia hawakumbuki ni nani waliyemuazimisha kabisa, ili kuepuka hili unahitaji kutunza kumbukumbu ya nani umemwazimisha kitabu au notes, ambapo utakuwa unaandika ni nani kaazima kutoka kwako na kaazima nini.

Ni muhimu kujua kuwa njia nzuri ya kuazima ni kukubaliana ni lini mwisho wa kutumia na kurejesha kwako. Na teknolojia rahisi huhitaji kuandika kwenye karatasi badala yake unaweza tumia vifaa vya digitali kuweka kumbukumbu zako.

# 3.

# Mkakati wa kurudia kusoma.

*"Chochote ulichosoma mara moja hakina uhakika wa kupata kukaa katika kumbukumbu ya muda mrefu mpaka utakapokirudia tena."*

Haijalishi uko vizuri kiasi gani, unahitaji kupata muda wa kurudia yale uliyosoma. Kurudia haimaanishi kutokuwa na akili lakini ni makakati wa kukusaidia kukuza uwezo wa akili. Kuna sababu nyingi ni kwa nini unahitaji kurudia kabla ya mtihani wa mwisho.

a) *Rudia kusisitiza*: Mara nyingi tunachosoma kinakaa katika kumbukumbu za muda mfupi mwanzoni na njia pekee ya kuzihamisha kwenda kwenye kumbukumbu za muda mrefu ni kupitia kurudia kusoma. Chochote ulichosoma mara moja hakina uhakika wa kupata kukaa katika kumbukumbu ya muda mrefu, unahitaji kuweka mkakati wa kuhamisha chochote ulichosoma kutoka utunzaji wa muda kwenda utunzaji kumbukumbu wa muda mrefu.

Hii inamaanisha kuwa hata ukifikiri umeelewa vizuri ambacho umesoma, kwa maana ya kutunza kumbukumbu za muda mrefu na uwezo wa kurudisha ulichosoma unahitaji kuandaa muda na kuwa na tabia ya kurudia mara kwa mara ulichosoma. Kwa hiyo kwa kila kozi ambayo unafanya hakikisha unaweka makakati wa kurudia mara kwa mara kabla hujakaa katika mtihani wako wa mwisho.

Mara zote unahitaji kuweka mchakato wa kurudia ambao unaweza kugawa katika sehemu ndogondogo kama kwa sura. Ili kuhakikisha kuwa unarudia yote yanayopaswa kusomwa kabla ya mtihani wa mwisho. Kuna nyakati ambazo kama hutakuwa na mpango mzuri wa kurudia utaweza kukaa katika mtihani na kufanya lakini utakosa pointi nyingi za kujibu na hata ukifanikiwa kujibu pointi zitakuwa hazina uzito.

b) *Rudia kukumbuka.* Sababu nyingine ya kurudia kusoma ni kukusaidia kukumbuka ambacho umesoma Jaribu kuangalia ulichosoma na kuona kama unaweza kukumbuka kirahisi (inaweza kuwa ni kanuni, nk).

Katika mpango makakati wa kurudia ndio wakati ambao utakuwa unafanya mazoezi kabla ya mtihani, hii inajumuisha kufanya marudio ya mitihani iliyopita au kufanya mazoezi yako binafsi na kuona umejiweka vipi kujibu maswali yatakapotokea katika mitihani.

Sasa unaweza kuandika chini kila kitu ambacho unakiona kuwa ni rahisi kusahau na weka mpango makusudi jinsi ya kuongeza uwezo wa kukumbuka. Kwa maneno mengine, Usirudie kusoma kwa mara ya pili kama vile ulivyosoma mara ya kwanza lakini fanya kwa namna fulani ya kutambua vitu muhimu na kujua sehemu ulizo

na udhaifu nazo katika kukumbuka na weka mpango mkakati kuhakikisha kuwa unausisitiza ubongo wako kukumbuka.

c) *Rudia kupanga mawazo vizuri*: Sababu nyingine ya kufanya marudio ni kukusaidia kuweka mawazo yako vizuri. Kama tu ilivyo kazi ngumu kutafuta kitu kwenye chumba ambacho kimepangwa hovyo, itakuwa kazi sana kwako kuweza kukumbuka kitu ulichosoma kama mawazo yako hayana mtiriko au mpangilio mzuri kwenye akili yako.

Kwa hiyo kufanya marudio ni namna pekee ya kupanga mawazo vizuri katika mtiririko mzuri. Kabla hujasoma weka mkakati wa kurudia katika namna ambayo ubongo wako utaweza kukumbuka sehemu tofauti tofauti ulizosoma.

Kumbuka kuwa kadri ya mawazo yako yalivyopangwa vizuri, ndivyo urahisi utakavyokuwa katika kujibu maswali. Usianze na chochote tu kufanya marudio, hakikisha umejipanga vizuri kabla ya kuanza.

Katika mpango makakti wa kurudia kusoma kuna vitu viwili unahitaji kujua:

***Moja*** ni kutumia asilimia 60 ya muda wako katika vitu ambavyo hauko vizuri navyo (bado hujavielewa sawa sawa) na Asilimia 40 katika vitu ambavyo umeelewa na unajua vizuri. Hii ni namna ya kujua wapi una uwezo napo vizuri na wapi una udhaifu kabla ya kuanza kufanya marudio. Usibadilishe asimilia ukaweka asilimia 40 kwenye vitu ambavyo hujaelewa na asilimia 60 kwenye vitu ambavyo umeelewa vizuri, kumbuka kurudia sio tu

inakusaidia kuelewa vizuri lakini inasisitiza kukumbuka ambacho umeshasoma.

***Pili*** ni kufahamu kuwa kuna hatua mbili tofauti na zote ni muhimu sana. Japo haijahakikishwa na sayansi lakini imekubalika kuwa mtu mmoja ana asilimia 80 ya kukumbuka kama atafanya marudio kwa vitu alivyosoma ndani ya saa 24. Hii ina maanisha kuwa unahitaji kufanya marudio mapema zaidi mara baada ya kufundishwa badala ya kusubiri kurudia kwa kutumia nguvu sana siku moja kabla ya mtihani. Kwa maneno mengine, njia rahisi ya kuongeza uwezo wa kukumbuka ni kupunguza muda kati ya ulipofundishwa na kurudia kusoma.

# 4.

# Mkakati wa kulala (kupumzika)

*"Usipo fanya bidii sana mwanzoni kabla ya mtihani, utakuwa na muda mchache sana wa kupumzika ukikaribia mitihani"*

Kiwango cha ulalaji siku chache kabla ya mtihani kinaweza kuwa na mchango hasi au chanya katika ubora wa ubongo wako kwenye kujibu mtihani. Hakikisha unapata muda wa kutosha wa kupumzika kabla ya mtihani.

Wakati unalala, ubongo wako unachukua zile taarifa ulizojifunza wakati unasoma, kwa hiyo kupata muda mzuri wa kupumzika utakusaidia kukumbuka vitu vidogo dogo vya msingi ulivyokuwa unasoma.

Ili kuhakikisha kuwa unaweza tumia usiku ili kupumzika vya kutosha siku kabla ya mtihani, unahitaji kutumia kanuni ya *TOIL- RELAX*. Hii ni kanuni rahisi tu nimeitumia na imefanya kazi vizuri. Inasema "Usipo fanya bidii sana mwanzoni kabla ya mtihani, utakuwa na

muda mchache sana wa kupumzika ukikaribia mitihani" Kwa hiyo unahitaji kuweka mpango makakati wa kusoma kwa bidii katika siku za mwanzoni mwa mhula wako ili uweze kutumia muda mdogo katika kurudia kipindi cha mtihani. Hii itakupa muda mzuri wa kuweza kupumzika.

Hii inawezekana kwa sababu katika vyuo vingi. Wiki za kwanza au miezi ya kwanza kunakuwa hakuna vipindi vingi na kazi nyingi. Unachohitaji kufanya ni kuwa makini katika wiki za kwanza ya masomo yako.

Kama utaweza kutangulia katika kozi yako na kukaa katika hali hiyo mwishowe utapata muda mzuri wa kupumzika na kusoma pasipo kuwa na presha ukikaribia mitihani yako. Lakini pia kama hukujiandaa vizuri na unakaribia mitihani hii inaweza kuwa sio ushauri mzuri kwako. Jaribu kutumia ushauri huu katika mtihani wako wa mhula ujao.

Kwa hiyo tengeneza ratiba yako ya kupumzika ili kuongeza uelewa, kumbuka kuwa muda wa kupumzika ni muda wa kuupa ubongo wako sura mpya, kadiri unavyopata muda wa kupumzika ndivyo akili yako inavyokuwa bora zaidi.

Naweza sema haishauriwi kukosa kabisa kupumzika usiku wa kuelekea mtihani. Wanafunzi wengi wanafikiri kusoma sana usiku kucha kutawasaidia kuwa bora lakini ukweli ni kuwa inaharibu sana uwezo wa ubongo wako. Unahitaji kuhakikisha kuwa kwa kila mtihani unaokaa kuufanya ubongo wako uko sawa na una nguvu. Kuingia kwenye mtihani ukiwa unajisikia usingizi na ubongo wako ukiwa umechoka kunaweza kuharibu utendaji kazi wako.

# 5.

# Mkakati wakupima uwezo wako

*"Mara nyingi watu huwa wanajikuta na tamaa ya kusoma vitu ambavyo wanaona kuwa ni rahisi, na wanavutiwa navyo lakini kwenye vitu ambavyo wanaona ugumu, si rahisi kuvipenda kwenye masomo yao"*

Jichunguze kujua hali yako kwa kila somo, ni zoezi muhimu katika kujiandaa na mitihani. Ukweli ni kuwa mkakati wa kujichunguza unatakiwa kuwa ndio muongozo katika mkakati wa kusoma kwa sababu hii itakusaidia kujua ni maeneo gani ambayo unahitaji kuwekeza zaidi na wapi ni rahisi kufanya marudio.

Kwa hiyo wiki chache kabla ya kuanza kufanya marudio unahitaji kuandika chini kozi zako zote halafu fanya

uchunguzi wa kweli na wa kina wapi ni rahisi kwako na wapi ni pagumu. Zoezi hili linapaswa kufanywa kwa kila sura katika kila somo unalofanya.

Namna rahisi niliyopata ya kufanya zoezi hili ni kuandaa kipimo cha kwanza (1) hadi cha kumi (10) na kisha andika namba kwa kila sura kwa somo moja ambapo (1 inaweza kuwa ni alama ya chini na 10 alama ya juu sana ya urahisi wa somo husika). Hii inamaanisha kuwa kila sura au somo ambalo linaangukia kwenye namba 1 hadi 5 yanahitaji muda zaidi na nguvu na kadiri namba zinavyoongezeka ndivyo unavyohitaji kuwekeza muda na nguvu kidogo. Kitu cha msingi kuhusu hili zoezi ni kuwa na tathmini binafsi (Hakuna mwingine wa kuweza kufanya zaidi yako).

Maswali yaafuatayo yanaweza kukusaidia kufanya zoezi hili

- Ni masomo yapi nina udhaifu au nguvu nayo? (andika)
- Ni maada gani katika somo husika nahitaji kuelewa zaidi?
- Nani anaweza kuwa msaada wa kutosha katika hili somo?
- Ni kitabu gani kinaweza kuwa rahisi kuelewa hii maada?
- Ni kanuni zipi ni rahisi kusahau na ninahitaji kuwa makini sana?

Mara nyingi watu huwa wanajikuta na tamaa ya kusoma vitu ambavyo wanaona kuwa ni rahisi kwao, wana raha

navyo na wanavutiwa navyo na kwenye vitu ambavyo wanaona ugumu, si rahisi kuvipenda kwenye masomo yao. Kufanya tathmini binafsi itakusaidia utakavyokuwa unarudia kusoma sio unasoma bila kupata kitu, zaidi sana ni mkakati mzuri katika masomo yako.

# 6.

# Mkakati wa makundi ya kujadiliana.

*"Kundi la kujadili ni moja kati ya mbinu ya kusoma, unahitaji kujiuliza baadhi ya maswali kabla ya kufanya maamuzi ya kujiunga katika kundi mojawapo."*

Makundi ya kujadiliana nayo ni mbinu nyingine ya kuongeza uelewa na kuongeza uwezekano wa kupata alama za juu. Pia usipokuwa makini makundi ya kujadili yanaweza kuwa ni chanzo cha KUPOTEZA MUDA, KUPEANA MSONGO WA MAWAZO, MTAZAMO MBOVU NA KUPOTEZA UELEWA SAHIHI.

Katika kusoma kuna aina tofauti za makundi ya kujadili kama ifuatavyo

## *Kundi la kufundishana*

Hili ni aina ya kundi ambapo kunakuwa na mtu mmoja ambaye anakuwa na uwezo zaidi ya wengine. Na kinachotokea ni kuwa mtu mmoja anawafundisha wengine wote kwa hiyo hata jina la kundi halipaswi kuitwa kundi la kujadili badala yake kundi la kufundishana.

Kwenye kundi la namna hii hakuna ushirikishwaji wa wanakundi wengine na kila mmoja anakuja kusikiliza na kufundishwa na hakuna mtu ambaye anafanya maandalizi kabla ya kukutana. Siku ambayo yule mtu hayupo basi kundi hili linaaghairisha kukutana.

Aina hii ya kundi linapendwa sana na wale wavivu kusoma na wanahitaji kupata tu walichofundishwa wengine. Kwa bahati mbaya yule anayekaririwa kuwa ndio bora wa kufundisha wengine anaweza wapoteza wenzake katika kuelewa, kwa sababu kila mmoja anafundisha anachokifahamu na kwa sababu hiyo anakaririwa kuwa na mamlaka ya kufundisha katika kundi, hakuna hata mmoja ambaye anathubutu kumpa changamoto anayefundisha hata kama hayuko sahihi.

## *Kundi la mabishano*

Katika aina hii ya kundi, ni mabishano tu hakuna mjadala. Katika aina ya kundi hili watu hawabishani juu ya pointi iliyotolewa lakini wanabishana juu ya nani katoa pointi. Muda mwingi katika kundi hili kunakuwa na pande mbili ndani yake ambazo wanakuwa kama washindani.

Ukiwa sehemu ya aina ya kundi hili, mara zote kunakuwa hakuna jibu ambalo limekubaliwa au kilichojadiliwa. Hii ni kwa sababu katika kundi hili watu hawajadili kuelewa au kufanya wengine waelewa lakini wanabishana kuwa washindi zaidi ya wenzao. Ni katika kundi hili ambapo unajikuta mnapoteza muda sana na kujikuta unaelewa kidogo sana.

### *Kundi la kupiga stori*

Aina nyingine ya kundi ni lile linalojulikana kwa kupiga stori ambazo hazihusiani kabisa na kinachojadiliwa mezani. Mara nyingi katika kundi hili watu wanaweza kuwa ni mashabiki wa mpira, muziki, wasanii au siasa.

Ukiwa kwenye kundi kama hili huwezi kuelewa kuwa hawa wanajadili masomo kwa ajili ya mtihani au wamekusanyika kujadili jambo lingine. Muda wa kujadili masomo unakuwa kidogo sana ukilinganisha na muda unaotumika kujadili mambo mengine yasiyohusiana na masomo.

Na hii inatokea wakati mjadala unaendelea mmoja wao anafungua mtandao wa kijamii na akiona kitu ambacho amekipenda anawaambia wenzake- “jamaa zangu tupumzike kidogo, hivi mmesikia hii?” mara atakaporuhusiwa kuleta stori yake kila mtu atataka kuunganisha na stori yake, wakati mnarudi kwenye mjadala tayari saa moja linakuwa limesha potea.

Kundi la kujadili ni moja kati ya mbinu ya kusoma, unahitaji kujiuliza baadhi ya maswali kabla ya kufanya maamuzi ya kujiunga katika kundi mojawapo. Baadhi ya maswali ya kukusaidia yameorodheshwa hapa chini:

- Swali la kwanza ni; Je nahitaji kweli kundi la kujadili muda huu? Baada ya kufanya uchunguzi yakinifu na tathmini binafsi ya kuelewa hali yako sasa unahitaji kuamua mwenyewe kuona kama kweli unahitaji kundi la kujadili la kuweza kukusaidia mahali ambapo ni dhaifu au la.
- Kitu cha pili unachohitaji kujiuliza ni kwa nini/ sababu ya kujiunga na kundi. "Nini ninahitaji kupata kutoka katika hili kundi?" (Kuelewa zaidi, kufanya maswali, kujadili maada ngumu, kupima uelewa kwa kutoa mchango wangu na kupokea kukosolewa, kuwafundisha ambao hawakuelewa ili kusisitiza katika akili yangu niweze kukumbuka na kuelewa zaidi? n.k). Hii itakusaidia kuchagua kundi ambalo unalihitaji na pia kujua kama unahitaji kuwepo katika kila mkusanyiko wa kundi lenu au la?

Ukishajiridhisha kwa mahitaji na sababu za kuwa mmoja katika kundi fulani, utahitaji kuweka jitahada kuhakikisha kuwa kundi unalohitaji linakuwa bora na kuleta mchango katika malengo kwa kuangalia yafuatayo:

- *Kukubaliana kanuni za kuwaongoza*
  Kitu cha kwanza cha kufanya kabla hamjaanza kujadili ni kuweka kanuni za kuwaongoza ambazo kila mmoja wenu atafuata.
  Baadhi ya kanuni muhimu ni pamoja na hizi – kufika kwa wakati mahali pa kukutania na kutoruhusu kuchelewa; kuchagua Kiongozi

wa kundi (inashauriwa kuwa na mtu zaidi ya mmoja – mnaweza kweka watu kutokana na siku au kwa kila somo na kuelezea nini majukumu ya kiongozi); kukubaliana juu ya matumizi ya simu na vitu vingine vya kielectroniki (mnawezakuamua kila simu iwekwe kimya au kuzimwa hadi mjadala utakapoisha au mkiwa na mapumziko katikati ya mjadala).

Kanuni zote hizi zitahakikisha kuwa mjadala uko katika mpango mzuri na wote wanaohusika kuwa na nidhamu na hivyo kuongeza thamani ya kupata kitu kutoka katika mjadala, hii itahakikisha ufanisi wa utumiaji muda wakati wa mjadala.

- *Kukubaliana juu ya ratiba na muda wa kutumia*

Hakuna kitu cha kupoteza muda kama hiki kwenda kwenye makundi ya kujadili na kuanza kufikiri nini cha kujadili. Mnahitaji kujadili na kukubaliana kama kundi nini cha kusoma na siku gani katika wiki husika, muwe na makubaliano ya pamoja kwa kila somo na nidhamu inahitajika muda wote. Kama kuna mabadiliko yanatakiwa kufanyika basi yaeleweke. Hii inahakikisha kuwa mnakuwa makini katika masomo na sio kukomaa na somo moja tu.

Kwa upande mwingine, unahitaji kukubaliana ni kwa muda gani mtatumia kujadili kila somo na kama mtakubaliana kujadili zaidi ya somo moja mnahitaji

kuweka wazi ni kwa namna gani mtaugawa muda kwa kila somo.

- *Kukubaliana njia ya kusoma*

Kama mlivyokubaliana kusoma kwa pamoja, mnahitaji kuweka wazi ni njia gani mtatumia kusoma. Hiyo njia inahitajika kueleweka na kila mmoja wenu. Baadhi ya njia za kusoma pamoja ni kusoma maada kwa kila somo ili kupata kila kitu. Hii ni kuhakikisha kila mtu anaelewa kila maada katika kila somo.

Njia nyingine ni kutumia maswali ya semina/ maswali ya mifano/maswali ya mitihani iliyopita na majaribio (tests) yaliyopita ambayo mwalimu wenu aliwapa kabla. Muda mwingi maswali hupima mtiririko wa mawazo au kukusaidia kuelewa. Kupitia maswali itasaidia kila mwana kundi kupata uelewa muhimu juu ya ufahamu fulani maalumu kukusaidia katika mitihani ijayo.

Njia nyingine ambayo inaweza kuwekwa katika kundi ni kwa kutumia muongozo wa kozi. Hii inahakikisha yote yanayohitajika kusomwa katika kipindi maalumu kwa kila somo yanakuwa yamesomwa vizuri.

Kwa namna yeyote, kama umeamua kufanya kundi la kujadili kuwa moja ya mbinu zako katika kusoma na kujiandaa na mtihani, hakikisha unafuata yote hapo juu kuwa na faida kutokana na hayo.

# 7.

# Mkakati wa kuchunguza mpangilio wa mtihani.

*"Jinsi akili yako ilivyojipanga kujibu na kuchagua maswali kabla ya kuingia katika chumba cha mtihani, ndivyo uwezo wa kukumbuka kuhusu maada husika unavyokuwa kubwa."*

Kuingia katika chumba cha mtihani bila kuwa na ufahamu mpangilio wa mtihani ni sababu nyinginne ya watu wengi kufeli. Kujiandaa vema bila kuelewe ni kitu gani unakwenda kukutana nacho ni kukuchanganya akili.

Kwa hiyo kabla ya kuingia katika chumba cha mtihani, ni muhimu kufahamu mpangilio wa mtihani wako. Mkakati wa kuchunguza mtihani unatakiwa uwe unaweza kuhusika na yafuatayo:

### *a) Mgawanyo wa sehemu za mtihani*

Kutokana na aina ya masomo yako, kila mtihani una sehemu zake husika. Mazoezi ni kwa kila sehemu kupitia

maada husika katika kozi. Kwa mfano, kuna sehemu katika mtihani ambayo inachukua mada mbili au tatu. Pia inahusisha uelewa yakinifu kwa kila sehemu ya mtihani na kutambua uwezo wako katika kila sehemu.

Kwa hiyo, badala ya kuwa mtu wa msaada kwa kila kitu na sio mhusika mkuu, mazoezi ya wanafunzi bora ni kuhakikisha kuwa wanaamua kabla ni maada zipi za kujibia mtihani na wanajiaandaa vizuri, kiasi kwamba swali lolote litakalo kuja kwenye mtihani basi wanaweza kujibu.

Hii inasaidia kukuweka makini utakapokuwa kwenye chumba cha mtihani na kupunguza kupoteza muda kufikiria swali lipi la kujibu (namna ya kuchagua maswali ya kujibu imeelezewa katika kitabu cha Siri ya Kupata alama juu ukiwa kwenye chumba cha mtihani). Jinsi akili yako ilivyojipanga kujibu na kuchagua maswali kabla ya kuingia katika chumba cha mtihani, ndivyo uwezo wa kukumbuka kuhusu maada husika unavyokuwa kubwa.

Katika kutambua mgawanyiko wa sehemu katika mtihani wako, inakupa kujua "maswali ambayo una uhuru nayo" hii ina maanisha sehemu zote ambazo una uelewa vizuri na upo tayari kujibu maswali bila shida yoyote. Kumbuka kuwa wote ambao wana ujasiri katika maswali fulani wana ujasiri ule wa ndani katika kukutana na maswali mengine katika mtihani.

### *b) Mgawanyo wa alama*

Weka mkakati katika muda wako wa maandalizi na kujizuia kutumia muda mwingi kwenye maada yenye maswali yanayotoa alama ndogo. Usiwe kama wanafunzi

ambao wanajua sana katika maada zenye maswali yenye alama ndogo na kujua kidogo kwenye maada zenye maswali yanayochukua alama nyingi. Uwingi wa alama unaonyesha uzito na umuhimu wa maada katika somo lako. Mambo mengi ambayo unahitaji kufahamu katika maada fulani huwa yanachukua uzito wa alama nyingi.

Kwa hiyo unapojiandaa kwa ajili ya mtihani, hakikisha unafahamu maada ambazo huchukua alama nyingi katika mtihani na jiandae kuongeza ufanisi katika maada hizo ambazo huchukua alama nyingi katika mtihani wako.

# 8.
# Mkakati wa kukumbuka

*"Njia nzuri ya kujua kuwa uko vizuri katika somo fulani tafuta mtu ambaye anahitaji kufudishwa na tengeneza muda wa utulivu wa kumfundisha."*

Hakuna kitu kinachoumiza kama kuingia katika chumba cha mtihani, na kuona maswali ambayo unajua umeyasoma lakini unashindwa kukumbuka chochote. Umeshawahi kuwa katika chumba cha mtihani na ghafla akili inapotea, haikumbuki kitu.

Kusahau mambo ni hali ya kawaida ya ubongo, lakini kusahau vitu ambavyo ulikuwa unatakiwa kukumbuka inasababisha shida sana na kukata tamaa.

Kwa hiyo kabla hujakaa kwenye mtihani, kumbuka kuwa na makakati wa kukumbuka wa kukusaidia kupunguza wingi wa taarifa ambazo unaweza kusahau wakati unazihitaji kufaulu mtihani.

Hatua ya kwanza katika mkakati wa kukumbuka ni kutambua taarifa zote muhimu ambazo ni rahisi

kusahaulika lakini unazihitaji katika akili yako. Baaadhi ya hizi taarifa zinajumuisha kanuni, michoro, majina n.k.

Lengo la mkakati wa kukumbuka ni kukusaidia kuvishika vitu vyote vya msingi ambavyo ni rahisi kusahaulika unapokuwa katika mtihani. Kama umekuwa ni mhanga wa kupotelewa na kumbukumbu katika mtihani, hii njia iliyothibitishwa itakuwa ni msaada mkubwa sana kwako.

Zifuatazo ni baadhi ya mbinu za haraka ambazo unaweza zitumia kuongeza uwezo wa kukumbuka.

### a) *Tafuta mtu wa kumfundisha*

Unapomfundisha mwingine ambacho umeelewa, ni njia ya kujifundisha mwenyewe mara ya pili, kumfundisha mwenzio sio kupoteza muda lakini ni kuwekeza katika ubora wako. Ukiwa unamfundisha mwenzako utakuja kugundua kuwa kuna maeneo ambayo yalikuwa ni magumu kwako kukumbuka na hivyo unausaidia ubongo wako uweze kutunza kumbukumbu ya kudumu kutokana na nguvu ya kurudia. Njia nzuri ya kujua kuwa uko vizuri katika somo fulani tafuta mtu ambaye anahitaji kufudishwa na tengeneza muda wa utulivu wa kumfundisha. Katika kufundisha utakugundua vitu vingi sana ambavyo vitakusaidia katika maandalizi yako ya mitihani. Jaribu kuangalia wanafunzi wanaofanya vizuri utagundua kuwa wapo tayari kufundisha wengine na kadri wanavyofundisha wengine ndivyo wanavyoongeza kupata ufaulu mzuri.

### b) *Tengeneza uhusiano*

Hujawahi ona kuwa mara zote ni rahisi kwako kusimulia stori fulani au muvi ulizoangalia zaidi ya habari nyingine? Ubongo wako umetengenezwa kwa namna ya kukumbuka kirahisi habari ambazo zimeunganishwa kuliko ambazo zinajitegemea kila moja pekee yake na hazina uhusiano wa pamoja.

Baadhi yenu bila shaka mtakuwa mnakumbuka jinsi tulivyokuwa tunaipa nguvu kumbukumbu yetu wakati tunakariri zile elementi kwenye somo la kemia, tutatungia wimbo na unaziimba, na huwezi sahau hata siku moja. Ubongo wako unakumbuka kirahisi chochote ambacho kimo katika stori au katika wimbo ambao unaunganisha hizo taarifa.

Uwezo wa kutengeneza muunganiko sio tu ni rahisi kukumbuka taarifa, lakini ni kama mafuta ya kuchochea ubunifu na akili. Steve Jobs mtu maarufu alisema “Ubunifu ni kuunganisha vitu. Ukiwa uliza wabunifu namna walivyofanya vitu vyao, wanajiona kama sio wabunifu kwa sababu hawajafanya kama watu wanavyoona, lakini waliona tu kitu fulani”

Kila mmoja anapenda kusoma na kusikiliza stori nzuri na kwa sababu njema tu – sio tu stori zinatufurahisha, bali zinatusaidia kuelewa na kukumbuka taarifa muhimu pia. Unaweza ukatumia hii katika masomo yako kwa kuweka taarifa muhimu katika mfumo wa stori.

### c) Tumia ramani na michoro

Ramani na michoro ni njia rahisi ya kuunganisha mawazo kwa kutengeneza muonekano wa tofauti. Unatumia muda kwa kutengeneza nadharia na picha

katika akili yako juu ya vile ulivyosoma kama vile unapofanya tafakari. Michoro itakusaidia kukumbuka na kuona picha katika akili yako ambayo itakusaidia kukumbuka katika chumba cha mtihani. Siku zote kumbuka hii, akili yako inakumbuka kirahisi vitu ambavyo vipo katika michoro zaidi ya kusoma na kusikia. Na hi ndio sababu ya kukumbuka vitu vingi ulivyoona wakati ulipokuwa mdogo kuliko ulivyosoma na kusikia. Kwa hiyo, kuwa na picha ya vitu ambavyo unataka kukumbuka vitakuongezea uwezo wa akili yako kukumbuka utakapo kuwa unahitaji.

### d) *Kitabu cha kumbukumbu/ubao wa kumbukumbu*

Hiki ni kitabu au ubao ambao umejitengenezea mwenyewe kwa ajili ya kupima uwezo wa kumbukumbu zako. Tafuta muda wa kuweza kufanya zoezi la kukumbuka kila taarifa ya muhimu (hususani zile ambazo ulikuwa unasahau sana), ziandike chini kwa usahihi wote na kisha fanya ukaguzi wako binafsi. Kama utatilia mkazo kufanya hili kwa kila taarifa ya muhimu ambayo ulikuwa unaogopa kusahau utaweza kupunguza upotevu wa taarifa zako katika ubongo wako katika kipindi cha mitihani.

### *e) Tumia kadi*

Hivi ni vipande vidogo vya karatasi ambavyo unaweza kuviweka katika meza, madaftari, katika ukuta n.k. Njia hii inaushughulisha ubongo wako ambao unaiwezesha kumbukumbu. Katika hiyo kadi kutakuwa na maneno muhimu ambayo yatakusaidia uweze kukumbuka taarifa nyingi kutoka kwenye neno moja. Sasa kwa kila eneo

ambalo unataka kuongeza uwezo wa kukumbuka, tengeneza kadi yenye dondoo za taarifa unazotaka kukumbuka, njia nzuri na yenye uhakika kuliko njia ya kusoma kawaida.

### f) *Pumzisha akili yako*

Wakati ubongo wako unafanya kazi, unahitaji kuwa unapata mapumziko mara kwa mara ili kuusaidia ubongo wako kuchukua taarifa za muhimu zote ulizosoma lakini pia kuupa hamasa na umakini wakati unafanya kazi.

Chukua mapumziko ya dk 45 – 50 lakini zaidi ya hapo umakini utapungua, chochote kipya baada ya saa moja na dakika 30 hakiwezi chukuliwa au kutunzwa vizuri na ubongo wako. Unaweza kusoma sana na kuchukua taarifa nyingi lakini hii inaharibu uwezo wako wa kukumbuka ulichosoma. Usiupe mzigo uwezo wako wa kukumbuka kwa tamaa yako ya kusoma mambo mengi. Kuwa smart!

# HITIMISHO

Hakuna somo gumu, na ni ukweli usiopingika kuwa kila somo kuna mtu au watu mahali fulani walifaulu kwa alama za juu sana, unaweza tumia kanuni zile zile katika masomo yako yote na itafanya kazi.

Mafanikio huacha alama, tunaweza kuwa bora kama wengine walivyofanikiwa. Kwenye kitabu hiki umesoma mbinu na jumbe ambazo zimewasaidia mamilioni ya watu kubadilisha taaluma zao, nawe utakapochukua hatua ya kuzitumia, wewe pia utapata mafanikio mazuri ya kitaaluma. Kumbuka hakuna mtu aliyezaliwa na akili ndogo, wote tuna nafasi ya kutumia ubora wetu wa akili kama tunajua ni namna gani ya kuongeza uwezo wetu. Kabla hujatua kitabu hiki andika mkakati wa kutekeleza kila ulichojifunza, Maamuzi yako ya kutumia mbinu hizi kwa vitendo ndiyo yatakayobadilisha taaluma yako. Anza leo usisubiri kesho.

# KUHUSU MWANDISHI

Joel Arthur Nanauka ni mwalimu anayefundisha sayansi ya maisha, kijana mwenye ushawishi mkubwa juu ya maendeleo kibinafsi, mkufunzi wa mashirika na mwandishi wa vitabu 20 vya Kiswahili, Kiingereza na Kifaransa.

Joel alichaguliwa kutoa mafunzo ya mwaka mmoja kwa vijana wajasiriamali wanaowania tuzo zilizoandaliwa na Benki ya BMCE iliyopo Casablanca Morocco. Mwaka 2019, Joel alitambuliwa na Avance Media iliyoko Ghana, kama kijana wa Kitanzania mwenye ushawishi mkubwa kwenye eneo la maendeleo binafsi na taaluma (Personal development and Academia) na alitajwa kwenye nafasi ya saba kama kijana mwenye ushawishi zaidi nchini Tanzania kwa ujumla.

Joel pia aliwahi kutajwa na Mkutano wa kimataifa wa uongozi wa vijana kama kiongozi bora wa vijana ulimwenguni nchini Taiwan-China mnamo mwaka 2002. Anatambuliwa na Graca Machel Trust (GMT) kama mshauri wa biashara kwa wanawake wajasiriamali. Mwaka 2019, Joel alikuwa mshauri mkuu wa biashara na usimamizi katika kufanya mabadiliko kwenye vituo vikuu

6 vya habari nchini Tanzania akivisaidia kufuata mfumo ulio bora wa ujasiriamali.

Mwaka 2018 alichaguliwa na Baraza la kitaifa la uwezeshaji wananchi kiuchumi (National Economic Empowerment Council) lililo chini ya ofisi ya Waziri Mkuu kuwa kwenye kamati ya ufundi ya kuandaa mwongozo wa mafunzo ya ujasiriamali kwa ajili ya biashara ndogo ndogo, za kati na kubwa.

Joel amepata elimu yake rasmi kwenye mambo ya usimamizi wa biashara (Bcom), maendeleo ya kimataifa, usimamizi wa miradi, uongozi na Diplomasia ya Uchumi na pia alishawahi kufanya kazi na Shirika la Umoja wa Mataifa (UNESCO) katika programu ya kimkakati kwenye sekta ya Elimu. Joel anajulikana kwa kutoa mafunzo yenye matokeo chanya katika mashirika ya kimataifa, mashirika ya kitaifa na mashirika muhimu ya serikali katika maeneo ya uongozi, usimamizi, biashara na utendaji wa kiwango cha juu sana.

Joel alikuwa mwanafunzi bora kitaifa kwenye mtihani wake wa kidato cha nne na mwanafunzi bora katika masomo yake baada ya kuhitimu Diplomasia ya Uchumi (Post-Graduate Studies in Economic Diplomacy).

Joel anaongoza kampuni inayotoa mafunzo mbalimbali ya Africa Success Academy (ASA) yenye ofisi zake jijini Dar es Salaam nchini Tanzania. Joel amemuoa Rachel na wamebarikiwa kuwa na watoto wawili wa kike, Joyous and Joyceline.

***VITABU VINGINE VILIVYOANDIKWA NA JOEL ARTHUR NANAUKA.***

**HARDCOPY (nakala ngumu)**

1. TIMIZA MALENGO YAKO (Mbinu60 walizotumia watu maarufukufanikiwa)
2. ISHI NDOTO YAKO (Siku 30 za kuishi maisha unayotamani)
3. TABIA 12 ZINAZOLETA MAFANIKIO
4. ISHINDE TABIA YA KUGHAIRISHA MAMBO
5. ONGEZA KIPATO CHAKO (Maarifa juu ya fedha, Biashara na uwekezaji)
6. NGUVU YA MWANAMKE
7. MBINU ZA KUFANIKISHA NDOTO KATIKATI YA CHANGAMOTO
8. HOW TO PASS YOUR EXAMS WITH EASE
9. UZALENGO NA UJENZI WA TAIFA.

10 UFANISI KAZINI

11 BORESHA MAHUSIANO YAKO

**SOFTCOPY (nakala ya electroniki).**

1. MONEY FORMULA (Elimu ya fedha isiyofundishwa shuleni)
2. HATUA SITA ZA KUJIAJIRI
3. MUONGOZO WA MAFANIKIO
4. CORE GENIUS (Jinsi ya kugundua uwezo wako wa kipekee)
5. JINSI YA KUFANIKIWA KATIKA NYAKATI NGUMU.
6. SAIKOLOJIA YA MTEJA
7. MBINU ZA KUJENGA UJASIRI NA KUJIAMINI
8. SURVIVING THE CRISIS.